

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

LEARNING BY EAR 2010

SHALL I TELL YOU SOMETHING?

AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 04: „THE HYENA, THE SNAKE, THE PANTHER AND THE WARTHOG“

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE

EDITOR: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAIMA GUIRA

TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS

PROOFREADING: TONY DUNHAM

KISUAHELI : ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (male, about 40 years old)
2. HYENA (female, about 20 years old)
3. WARTHOG (male, about 30 years old)
4. WHITE-BEARDED OLD MAN (male, sounding +/- 70 years old)

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

INTRO / PRESENTER:

Hujambo msikilizaji na karibu kwa makala ya nne kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo! Jenga Maisha yako vinavyotayarishwa na Deutsche Welle. Tukiwa bado tunasimulia ngano za utamaduni wa Mwafrika kuhusu mbinu za kutatua mizozo na kudumisha amani, katika maada "Je nikudokezee?" Je, mara ya mwisho kusikiliza ngano za vichimbakazi ilikuwa lini? Jana usiku? Wiki mbili zilizopita au miaka?

Mara nyingi ngano huwa hadithi zinazotumiwa kufafafanua ukweli halisi wa mambo duniani. Hata hivyo lakini ngano hizi huweza baadaye kuwafungua macho wengi na kuwaondolea ujinga. Kama ujuavyo, watu wanapoishi kwa pamoja na kutangamana huwa na uwezo mkubwa wa kubuni nyezo za kustawisha maendeleo.

Hivyo basi ngano tunayoizungumzia hii leo, inahusu mbinu muafaka za kukabiliana na mizozo mbali na kuleta maridhiano miongoni mwa jamii.

Yaani ni vipi unaweza kukabiliana na hali ngumu maishani? Au vipi unavyoweza kukabiliana na ukosefu wa imani, wivu, uchoyo na ubinafsi?

Katika kila ngano au hadhithi, mtu hakosi kujifunza jambo moja au mawili ambayo yanaweza kumsaidia maishani.

Hivyo endelea kusikiliza ufahamu kwanini fisi aliadhibiwa kwa ulafi wake katika ngano hii ya Fisi, Nyoka na Ngiri".

1. MUSIC (*play as background for the entire script*)

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

2. NARRATOR:

Hapo zamani za kale palitokea Fisi, Nyoka, Chui na Ngiri. Wanyama hawa walipindukia kupendana sana na hata kumiliki shamba kubwa kwa pamoja. Lakini marafiki hawa wakubwa, walikuwa wakijitegemea kwa chakula. Na tabia hiyo ikaendelea kwa muda mrefu!

Lakini siku moja wazo likamjia Fisi na kupendekeza mfumo rahisi ambao ulikubaliwa na wote. Kwamba kuwe na utaratibu wa zamu kutafuta chakula cha kuwatosha wote kwa muda wa wiki nzima. Lakini siku iliyofuatia, Fisi akaongeza kipengele kingine katika muafaka huo:

3. HYENA:

"Na yule atakayeshindwa kuleta nyama ya kututosha sote watatu, tutamlal yeye!"

4. NARRATOR:

Wazo hili liliridhiwa na wote.

Na wiki ya kwanza ikawa zamu ya nyoka. Akaenda kuwinda kichakani. Akiwa kichakani alitumia meno yake yenye simu kali kumng'ata kila mnyama aliyekutana naye.!

5. SFX: *Snake slithering and hissing*

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

6. NARRATOR:

Na alirudi nyumbani na nyama nyingi, akatayarisha chakula cha kuwatoshaleza wote watatu. Marafiki hao walikula shibe yao kwa furaha na wala hawakuweza kukimaliza chakula hicho.

Wiki ya pili ,ikawa zamu ya Chui. Jioni hiyo alijificha kichakani kando kando ya mto kuwavizia wanyama wote waliokuja kunywa maji mtoni. Pia alirudi nyumbani na chakula cha kuwatoshya marafiki zake. Matumbo yao yalivimba kutokana na kushiba na hata kushindwa kufanya kazi siku iliyofuatia.

Wiki ya tatu ikwa zamu ya Fisi.

7. SFX: *Laugh of the hyena*

8. NARRATOR:

Giza lilipoingia, Fisi na tabia yake ya ibilisi alienda kuiba vipande nya nyama vilivyosazwa na wanayama wengine. Kisha akaviburuta hadi nyumbani kwao. Lakini mizoga hii ambayo ni mabaki ya chakula cha Simba na makurumbembe ilikuwa ikitoa mvundo mkali na wanyama wengine hawakufurahia chakula hicho.

Wiki ya nne iliingia na ikawa zamu ya Ngiri.

Kwa namna Fisi alivyokuwa akimtazama Ngiri kwa shauku, Ngiri alishikwa na wasiwasi lakini akiendelea kuramba kipande cha nyama aliyokuwa akila.

Fisi alikuwa na hakika kwamba Ngiri hatafaulu kuleta chakula chochote kutoka mawindoni.

Je, umewahi kumuona Ngiri akiwinda?

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

Na Fisi alipokutana na Ngiri baada ya chakula, alitikisa kichwa tu kwa kumuhurumia Ngiri.

9. HYENA:

"Oh maskini rafiki yangu Ngiri!"

10. NARRATOR:

Kisha akageuza uso wake kuficha kicheko cha kejeli dhidi ya Ngiri.

11. SFX: *Laugh of the hyena*

12. NARRATOR:

Kitendo hicho kilimfanya ngiri kuingiwa na mawazo mengi sana. Na kisha baadaye akafahamu kwanini Fisi akawa na tabia hii ngeni.

13. WARTHOG:

"Ah! Kumbe fisi alifahamu vyema udhaifu wangu tangu mwanzoni na ndio sababu ya kuongeza kipengele cha pili kwenye makubaliano haya!"

14. SFX: *Echo Hyena*

"Yeyote atakayeshindwa kuleta chakula cha kututosha sote tutamfanya kitowe,!“ akakumbuka.

15. NARRATOR:

Basi huku akiwa mwenye wasiwasi na kukata tamaa, Ngiri alitapatapa kama mwendawazimu kutafuta chakula cha kuwatoshua

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

wote wanne.

16. SFX : *Scurry and grunting warthog*

17. NARRATOR:

Maskini Ngiri, juhudzi zake ziliambulia patupu kwani kila mnyama
aliyemvizia alikuwa mwerevu zaidi kuliko yeye. Na mwishowe
akakata tamaa:

18. WARTHOG:

"Sina bahati! Oh! Maskini sina bahati kabisa leo!"

19. NARRATOR:

Ghafla akamuona Mzee mwenye ndevu kubwa ambaye
alishangazwa na Ngiri huyu aliyeonekana mwenye wasiwasi na
kukata tamaa.

20. WHITE-BEARDED OLD MAN:

"Una shida gani Kaka Ngiri? Kwanini unalia? Unaugua?"

21. NARRATOR:

Akinung'unika, Ngiri kisha akamweleza masaibu yake kwa sauti ya
kulalama.

Yule mzee ambaye alikuwa kama mganga akamuonea huruma na
kukubali kumsaidia. Alitia mkono mfukoni na kutoka kipande cha jiwe
lenye kumeremeta, akampa Ngiri na kisha akamwambia:

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

22. WHITE-BEARDED OLD MAN:

"Wakati unapokutana na mnyama yoyote unayetaka kumuua, lishike
jiwe hili mbele yake na kusema maneno haya:
Ewe jiwe la miujiza! Ewe jiwe la miujiza!
Tafadhalii nisaidie!.

Na jiwe hili litaitikia kilio chako. Na kisha utasikia ngurumo kama
radi...

23. SFX: *Thunderbolt*

24. NARRATOR:

... kisha mnyama huyo ataanguka na kufa papo hapo. Baadaye
utahitajika kulibembeleza na kulisifu jiwe hili ili nguvu zake zisije
kukugeukia:

Kwa kusema tena maneno haya:

*"ewe jiwe la miujiza, ewe jiwe la miujiza! Ama kwa hakika uwezo
wako ni wa kustaajabisha".*

25. NARRATOR:

Ngiri alimshukuru sana mzee huyo na kisha moja kwa moja
akarejea mawindoni kurajibu bahati na jiwe lile la miujiza.

26. SFX: *Thunderbolt*

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

27. NARRATOR:

Akiwa njiani alifafulu kuua wanyama na ndege wengi na hivyo
kuepukana na hatari ya kuuawa na rafiki zake nyumbani. Kweli
mzee yule alimwambia ukweli kwani yote aliyomuahidi yalitimia!
Wakati rafiki zake walipomuona amebeba mzigo mkubwa wa
mizoga walishangaa sana hasa Nyoka na Fisi ambao walitilia shaka
uwezo wake wa kuleta chakula cha kutosha nyumbani. Wiki hiyo
walifurahia chakula kizuri na kumsifu Ngiri kama mfalme.

28. SFX: *Animals eating*

29. NARRATOR:

Kisha kwa janja zake, mara kwa mara Fisi alitaka kuandamana na
Ngiri kila anapokwenda kuwinda. Lakini Ngiri hakutaka Fisi ajue siri
yake, jambo lililomkasirisha sana Fisi.

Baada ya wiki tatu hivi, ikafika tena zamu ya Ngiri kwenda
mawindoni. Huyo akaelekea kichakani bila ya kufahamu kwamba
Fisi alikuwa akimfuata nyuma. Fisi alimnyapia Ngiri kichakani na
hapo akagundua siri ya jiwe lake la miujiza.

30. WARTHOG:

*"Ewe jiwe la miujiza, Ewe jiwe la miujiza!
Tafadhalii nisaidie, ewe jiwe la miujiza."*

31. SFX: *Thunderbolt*

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

32. NARRATOR:

Fisi alisikia maneno hayo na akawa amefaulu kupata siri ya Ngiri.

Lakini kwa pupa akarejea nyumbani mbio bila ya kufahamu kwamba kulikuwa na sehemu ya pili ya siri baada ya kufanikiwa unachokitaka, yaani kutoa shukrani kwa jiwe hilo.

Asubuhi, wakati walipokuwa wakitoka kwenda shambani, Fisi alilalamika kuugua huku akigagaa mchangani kwa uchungu.

Lakini Ngiri hakumuamini rafiki yake. Aliona kama ni ujanja wake asiende kufanya kazi shambani! Na kweli, punde tu Fisi alirudi nyumbani alianza kuchakura kila pembe na hatimaye kuliiba jiwe lile. Huyo akaingia kichakani kuanza kuwinda. Mnyama wa kwanza kumuona alikuwa Paa na bila ya kupoteza wakati akalitoa jiwe na kutumia mbinu ile ya rafiki yake..

"Ewe jiwe la miujiza, Ewe jiwe la miujiza!

Tafadhal nisaidie, ewe jiwe la miujiza."

Kisha Paa akaanguka na kufa papo hapo. Lakini mtihani mkubwa ulikuwa maneno ya mwisho kutoa shukrani kwa jiwe lile. Jiwe likasubiri na kusubiri lakini wapi! Na hapo jiwe likakasirika na kuanza kutoa moto. Licha ya juhudzi za Fisi kutaka kulitupa jiwe lile lilimganda kwenye viganja vyake na kuendelea kumchoma hali iliyomuogofya Fisi. Basi Fisi alitapatapa na kupiga makelele lakini wapi!

33. SFX: HYENA howling

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

34. HYENA:

"Niache niende nyumbani wewe jiwe la miujiza, kwenda, kwenda kabisa!"

35. NARRATOR:

Maskini hakujuua kwamba jiwe hilo lingeweza kusikia tu maneno yale ya siri alijoambiwa Ngiri. Fisi alishikwa na wasiwasi asijue la kufanya.

36. SFX: HYENA howling

37. NARRATOR:

Na kilio chake kikawashtua wanyama wengine waliokuwa mbali sana na eneo hilo, huku akikimbilia shambani ambako amewaaacha wenzake wakifanya kazi. Walipomuona fisi hawakumuamini, walidhani labda amezidiwa na tumbo lake lililokuwa likimuumma. Lakini ndio mwanzo akazidisha kilio. Ngiri kuona viganja vyake vinateketea mara moja akafahamu yaliyomkuta. Alianza kumcheka huku akimuonea huruma. Ngiri kwa sauti ya chini alitamka yale maneno alijoambiwa na Mzee:

38. WARTHOG:

"ewe jiwe la miujiza, ewe jiwe la miujiza!Kwa kweli uwezo wako ni wa kustaajabisha".

39. NARRATOR:

Na hapo viganja vyaa Fisi vikafunguka na jiwe likaanguka miguuni mwa Ngiri.

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'

Episode: 04 The hyena, the snake, the panther and the warthog

Author: Ibrahima Ndiaye

40. **SFX: Dull sound of a falling stone**

41. **NARRATOR:**

Kwa mshangao wa Nyoka na Chui, Ngiri alilichukua jiwe lile bila ya hata woga wowote wa kuteketeza vidole vyake.

Na tangu wakati huo, wanyama wengine walimheshimu sana Ngiri kama mnyama mwenye busara.

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na atajaye kuwa wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.

42. **Music**

OUTRO:

Na hadi hapo tunafika mwisho wa ngano yetu leo. Lakini je, umewahi kushuhudia kisa cha miujiza ya kuleta baraka kama jiwe hili? Au hizrizi uanayobeba mfukoni kila unakokwenda?

Tufahamishe kupitia email yetu lbe@dw-world.de.

Na ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki au vipindi vingine vya Noa Bongo tembelea mtandano wetu wa www.dw-world.de/lbe.

Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa.

END